**TAARIFA YA HUDUMA ZA VIJANA, CHAPLENSIA, NA MUZIKI KUANZIA 2023 MPAKA 2025**

"Jeshi la watendakazi kama vijana wetu, wakifunzwa vema,wakitengenezwa vizuri, ni kwa haraka kiasi gani ujumbe wa kuangikwa, kufufuka, na kurudi kwa Mwokozi kwa haraka kutachukuliwa kwa ulimwengu!" MYP 196.

**Yaliyomo**


A. UTANGULIZI
B. MALENGO MAKUU YA IDARA YA HUDUMA ZA VIJANA
C. MIKAKATI ILIYOTUMIKA KUFANIKISHA MALENGO HAYA MAKUU
D. BAADHI YA MATUKIO KATIKA PICHA
E. HALI YA IDARA KWA UFUPI
F. CHANGAMOTO ZA IDARA
G. MAPENDEKEZO KWA UONGOZI UJAO ILI KUKABIIANA NA CHANGAMOTO HIZI
H. MALENGO YA IDARA 2025-2030


## A. UTANGULIZI

Natumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya uongozi Wake na mibaraka Yake kwa miaka hii mitatu 2023-2025. Taarifa hii inatuonyesha michango ya viongozi wa vijana makanisa mahalia, wazazi wa vijana wenyewe, washiriki wa makanisa katika kuongoza na kuwalea vijana wa Kiadventista walioko majumbani mwetu, mashuleni na makanisani kwa kipindi hiki cha miaka mitatu. Taarifa hii vilevile itatoa mafanikio kwa ufupi, changamoto na mapendekezo kwa miaka mingine mitano ijayo kwa neema ya Mungu, 2025-2030.

Siyo kazi rahisi sana kuongoza jeshi hili kubwa la vijana katika kanisa la Mungu na kufikia kutoa taarifa. Yapo mengi ya kukumbukwa, ila yapo yasiyoweza kusahauliwa (1) Kulala porini kwa siku 12 kila mwaka kwa miaka mitatu na nyoka na nge wasikushughulikie, vijana wote watoke salama na kurudi majumbani mwao. Hakika ni mkono wa Mungu siyo ujanja wa mwanadamu. (2) Kupambana na tembo kila kona na kutoka salama kwa mkono wa Mungu (Kuona vijana wakizimia kwa mistuko ya heka heka za kambi na wakizinduka tena na kuendelea na kambi, inahitaji huruma za Mwenyezi Mungu na uongozi wa Roho Mtakatifu kuondoa hofu na mashaka wala siyo ujuzi wa madaktari. (3) Kukubalika kwa wanakijiji mahali kambi lilipo na kutoka kwa amani wakiwa wamefurahi na kuomba mrudi tena. (4) Kwenda kambini ukiwa na Tshs 33,000 tu kisha Mungu Afanye muujiza wa kuleta wanakambi na utoke bila deni, inahitaji kuongezewa Imani vinginevyo unaahirisha mkutano dakika za mwisho.

Kwa hayo yote nasema tena Jina la Bwana Yesu na lipewe sifa.

## B. MALENGO MAKUU YA IDARA YA HUDUMA ZA VIJANA

1. Kuwapatia vijana misingi ya Kibiblia
2. Kuinua maisha ya sala ya kijana
3. Kuwaongoza vijana kufahamu uthamani wao binafsi na kugundua na kuendeleza vipawa vyao vya Roho na uwezo yao
4. Kuwawezesha na kuwapa vijana uwezo kwa maisha ya kutumika
5. Kuwafundisha vijana kanuni za uwakili
6. Kuhakikisha kuwaingiza vijana katika Nyanja zote za maisha ya kanisa na uongozi

## C. MIKAKATI ILIYOTUMIKA KUFANIKISHA MALENGO HAYA MAKUU 2023-2025

Ili kufanikisha malengo haya makuu, Idara ya huduma za vijana Kanda ya Kaskazini Mashariki mwa Tanzania iliunda mipango mkakati ifuatayo:-

a) Malengo ya Ukuaji Kiroho.
    1. Kuwafanya vijana na familia zao kuwa wafuasi kwa kujazwa na Roho Mtakatifu katika maisha yao kutoka 68% hadi 80% kutoka mwaka 2023 na kuendelea kwa kuongeza 6% kila robo
    2. Kuongeza kiwango cha kuwafanya vijana wasiliasi kanisa na ushiriki wa vijana na familia zao kutoka 40% hadi 98% kuanzia mwaka 2023 na kuendelea
    3. Kuwasaidia vijana kumweka Mungu Kwanza na kuonyesha mfano wa maisha ya Kibiblia kwa mtazamo wa ulimwengu kutoka 43% hadi 86% kuanzia mwaka 2023 na kuendelea

b) Malengo ya Kiuongozi
    1. Kuimarisha wajibu wa uongozi wa Waratibu wa maeneo (Area coordinators), viongozi wa vijana makanisa mahalia, wachungaji na wengine walio mstari wa mbele kuwategemeza vijana na kuwapatia fursa za mara kwa mara kwa ukuaji wa vijana kuanzia mwaka 2023 hadi September 2025 na kuendelea
    2. Kuhakikisha kuwa rasilimali za kanisa zinatumika kulingana na mipango mkakati ya Konferensi kutoka 3% hadi 99% ifikapo September 2025 na kuendelea

c) Malengo ya Kimishenari
    1. Kuamsha wazo la umishenari na kujitoa kafara kwa ajili ya umishenari kama njia ya maisha yote kwa kuwahusisha siyo wachungaji tu bali na vijana vile vile katika hali ya kushuhudia kwa furaha kwa ajili ya Kristo na kufanya wafuasi mara mbili kila mwaka kuanzia Januari 2023 na kuendelea.

Ili kufanikisha haya malengo Idara ya huduma za vijana kanda ya Kaskazini Mashariki mwa Tanzania ilifanikiwa kufanya haya yafuatayo kwa miaka hii mitatu.

1. Idara iliendesha semina za uongozi kwa viongozi wa vijana, wachungaji, wazee wa makanisa na washiriki kila mwanzoni mwa mwaka kwa miaka yote mitatu, ili kukuza uwezo wa kiuongozi kwa viongozi wa kanisa kwa ajili ya huduma na malezi ya vijana.
2. Kutembelea mitaa kadhaa kwa ajili ya semina hizi za uongozi na uamsho
3. Vijana waliendesha mikutano ya hadhara na kuongoa roho
4. Vijana wa TUCASSA walihudhuria mikutano ya mwaka ya union, Tabora na Mwanza
5. Vijana walihudhuria kongresi ya union Tabora na kambi la vijana Bunda
6. Idara ilifanikiwa kuendesha makambi ya mafunzo kwa vijana kila mwaka kwa miaka mitatu, na vijana walivishwa pini, nishani na semina mbalimbali
7. Mpaka sasa Konferensi nzima tuna MG 478 waliofaulu na SYL 60 waliofaulu, kati yao wachungaji walivishwa pini ya MG na wengine SYL. Hili limeongeza idadi ya viongozi wa vijana waliopata semina za uongozi wa vijana.
8. Vijana walifaulu kufanya matendo ya huruma kila mwaka kwa kutoa vitu mbalimbali kwa wahitaji na kuchangia damu.
9. Huduma kwa magereza yaliyopo kwa konferensi imeongezeka, mpaka sasa magereza 3 yanahudumiwa na makanisa. Same, Handeni na Maweni. Mipango inafanywa ili kufungua kazi kwa magereza mengine. Jumla kwa conference tuna magereza 13
10. Vijana wa TUCASSA na ASSA wameendelea kuendesha mikutano yao kikanda na kufanya mahafali kwa kushirikiana na baadhi ya makanisa. Jumla kwa conference tuna shule za sekondari 385 na shule za msingi 772, na vyuo vikuu na kati 56.

**D. BAADHI YA MATUKIO KATIKA PICHA**



MWENYEKITI WA CONFERENCE PR. NZUMBI AKIVISHA PINI SYL



KWAYA YA GETHSEMANE WAKIWA EFFORT MAHIDA- ROMBO




VIJANA MTAA WA MABAWA WAKIKABIDHI VIFAA GEREZA LA MAWENI



SIKU YA WATAFUTANJIA DUNIANI TANGA




UVISHAJI WA PINI YA SYL CONGRESS YA UNION, MWENYEKITI NETC PASTO NZUMBI AKIWEPO, KUVISHWA NA KUVISHA WAHITIMU- TABORA



MWENYKITI WA CONFERENCE AKIWA NA MKURUGENZI WA VIJANA ECD, NTUC SIKU YA MATENDO YA HURUMA KISIMA- SAME 2024



KAMBI LA VIJANA KANDA YA KILIMANJARO- TPC 2024



KAMBI TPC MOSHI- KAMBI LA VIJANA KWENYE NISHANI



KAMBI TPC NISHANI YA UJENZI

**E. HALI YA IDARA KWA UFUPI**

**Jumla conference tuna washiriki __81,802_ Vijana waliopo kwa conference (4-30) 56,795**

| IDADI YA MAKANISA: 416 | VIJANA WADOGO | | VIJANA WAKUBWA | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| **IDADI YA MAKUNDI: 152** | **(4-15)** | | **(16-30)** | | |
| | **A.C. (4-9)** | **P.F.C (10-15)** | **A.M.C. (16-21)** | **Y.A. (22-30)** | |
| **MUUNDO** | | | | | |
| Vyama vilivyopo | 401 | 403 | 405 | 405 | 1,614 |
| Wanachama kwa chama | 7,113 | 13,452 | 11,697 | 8,934 | 41,196 |
| Waliobatizwa kwa chama | - | 5,687 | 10,169 | 6,941 | 22,797 |
| MAFUNZO YA UONGOZI | | | | | |
| Walioshiriki mafunzo ya uongozi kwa ujumla | 3,457 | 2,578 | 2,681 | 2,156 | 10,872 |
| Wachungaji, Wazee na viongozi waliofunzwa AYMT | 953 | 1,269 | 943 | 894 | 4,059 |
| MG Waliopo | | | | | 478 |
| Waliopata vyeti vya AYMT | | | | | 692 |
| SYL Waliopo | | | | | 60 |
| **UANAFUNZI** | **AC** | **PF** | **MABALOZI** | **YA** | **JUMLA** |
| Wanaoshiriki kusoma Biblia kwa mpango | 2,467 | 7,941 | 6,529 | 6,947 | 23,884 |
| Wanaofanya kesha la asubuhi | 2,358 | 2,563 | 5,841 | 6,901 | 17,663 |
| Wanaosoma vitabu vya Roho ya Unabii | 1,013 | 2,157 | 1,853 | 3,902 | 8,925 |
| Wanaosoma vitabu vya Chama vilivyoagizwa | 578 | 2,465 | 2,138 | 1,684 | 6,865 |

**F. CHANGAMOTO ZA IDARA**

**1. HUDUMA ZA VIJANA.**

Bado kuna makanisa hayana vyama vilivyo hai na yapo makanisa ambayo hayana MG, NA SYL waliofaulu. Hii ina maana kuwa hawana viongozi wanaoweza kuendeleza maswala ya uongozi wa vijana kanisani. MG, NA SYL wengine waliofaulu hawako hai makanisani. Wakishavishwa wanalala hawalisaidii kanisa tena. Wapo MG waliofaulu zamani wakati wa MV sasa ni wazee hawawezi tena kukimbizana na vijana kwa mafunzo yao. Wazee wengi wanaochaguliwa kanisani hawana elimu ya namna ya kuongoza Idara ya huduma za vijana.

2. **CHAPLENSIA**

Kuna tatizo la makanisa mengi kutohudumia mashule au taasisi za umma kwa shule za msingi na sekondari. Vilevile kwenye vyuo vikuu na vya kati makanisa mengi wanaogopa kuwahudumia vijana wetu walio kwenye hizi taasisi. Shule zetu za kanisa hazijakuwa na vyama vya vijana vilivyo hai, wanafundisha tu masomo ya dini na kuingiza ibada ila masomo ya miongozo ya Idara ya huduma za vijana bado zinahitaji uamsho mpya. Makanisa mengine hayachagui Waratibu wa taasisi za huduma za umma (PCM) Hivyo vijana wetu kukosa malezi sahihi ya kanisa kando ya kupewa vyeti tu vya mahafali wakati hawajafundishwa cho chote cha kulijua kanisa.

3. **MUZIKI**

Kwaya za makanisa zimeendelea kutoa huduma mbalimbali za uimbaji kwa mikutano na semina mbalimbali. Bado kuna tatizo la muziki wa ibada. Kwaya nyingi bado wanaimbia ngoma zisizokubalika kwa ibada. Tatizo ni waalimu wa kwaya kukosa utaalamu wa muziki. Ili kutatua tatizo hili kunahitajika kuwa na masomo ya muziki kwa waalimu wote wa kwaya makanisani.

**G. MAPENDEKEZO YA UFUMBUZI KWA CHANGAMOTO HIZI.**

1. Kuhakikisha kuwa kila kanisa kwa muhula ujao linakuwa na Huduma za vijana zilizo hai. Kuandaa viongozi wa vijana makanisani ambao watapata kozi za MG, na SYL. Ikiwa ni Pamoja na wachungaji waliobaki kupata kozi hizi.
2. Kuendesha kambi la conference la MG na SYL waliohitimu na mafunzoni
3. Kuhakikisha kuwa kila shule na chuo katika eneo la kanisa husika pamoja na gereza vinahudumiwa kikamilifu kwa malezi ya kiroho na uongoaji roho
4. Mkurugenzi wa Elimu conference kuhakikisha miongozo ya kufundishia somo la dini mashuleni inapatikana kwa kila kanisa.
5. Kuwa na semina ya muziki kwa waalimu wa muziki makanisani kwa kuleta wataalamu wa muziki na kukamilisha kozi hiyo kwa muhula ujao ili kuondoa tatizo la utaalamu wa muziki makanisani kwa conference yote.

**H. MALENGO YA MIAKA MITANO IJAYO 2025-2030**

Kwa nguvu na mamlaka ya Roho Mtakatifu, Idara ya huduma za vijana NETC itazingatia juu ya vipaumbele vinne vya mikakati:-

1. **USHIRIKA NA MUNGU**
2. **UTAMBULISHO KATIKA KRISTO**
3. **UMOJA KUPITIA ROHO MTAKATIFU**
4. **UTUME KWA WOTE]**

### USHIRIKA NA MUNGU

Lengo: Vijana watakua kufikia ufuasi uliokomaa wa kiroho kwa kuwa na mahusiano na Mungu kila siku kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu , uhusiano wa kina Pamoja Naye kwa kuwa na maombi ya kila siku, kujifunza Biblia, utume kwa huduma ya uwakili mwaminifu, na kuingiza katika maisha ya kila siku maelekezo ya uvuvio wa Roho ya Unabii, kutoka 58% hadi 90% ifikapo Septemba 2030 kwa kuongeza 6% kila mwaka.

### UTAMBULISHO KATIKA KRISTO

Lengo: Kuthibitisha utambulisho wa vijana kama Watoto wa Mungu, vijana watakuwa hai katika Kristo, wakikita Imani yao na kukua katika Imani na kweli, kwa kutunza amri za Mungu, kutafuta mambo ya juu na kuzaa matunda katika kila kazi njema. Kupitia kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, vijana watasonga mbele wakiungana Pamoja katika upendo, wakihubiri injili ya milele kwa maeneo yote ya conference na ulimwengu kwa ujumla, wakikazia ujumbe wa tumaini wa unabii wa siku za mwisho. Kutoka 60% hadi 85% ifikapo Septemba 2030 kwa kuongeza 5% kila mwaka.

### UMOJA KUPITIA ROHO MTAKATIFU

Lengo: Vijana wanaunganishwa katika mwili wa Kristo kupitia Roho Mtakatifu. Wataonyesha umoja wao kupitia kulifundisha Neno, kupendana wenyewe, ibada, kushuhudia, kuwahudumia wengine, na kujiandaa kwa Mvua ya Masika ya Roho Mtakatifu. Wataungana na kanisa la ulimwengu kwa kutoa ujumbe wa unabii wa Ufunuo 14:6-12 na ujumbe wa Kristo wa upatanisho kwa matarajio ya marejeo yake ya mara ya pili kutoka 55% hadi 80% ifikapo Septemba 2023 kwa kuongeza 5% kila mwaka

### UTUME KWA WOTE

Lengo: Kwa kuwezeshwa na kupewa nguvu na Roho Mtakatifu, Vijana wote wa NETC na taasisi zake watashiriki kila mmoja binafsi katika kutangaza injili ya milele kwa kila eneo la NETC, makabila yote, wilaya zote kata zote na vijiji vyote na watu wote. Agizo la kufanya wanafunzi linahitaji mbinu za kisasa wakati tukiendelea kuwa wa kweli kwa Kristo kuchukua hali ya ubinadamu na kutumia mbinu zote katika utume. Vijana watachangamana kama Kristo alivyochangamana, kuonyesha huruma, kuwasaidia wahitaji na kujenga tumaini kwao kama Yesu alivyofanya. Vijana watawaongoza watu kwa mwaliko wa Yesu Kristo wa kuwa wafuasi Wake na kujiunga na kanisa Lake la Waadventista wa Sabato kama wafuasi wake wanaofanya wafuasi kwa kushirikiana na takwimu za Mratibu wa maeneo mapya ya NETC.

Imeandaliwa na kuletwa kwenu na

Mchungaji John Kimbute

Mkurugenzi Huduma za Vijana 2023-2025